



# Sustainable Development Goals (SDGs) BOOK CLUB AFRICAN CHAPTER

**Kiswahili Reading List: SDG 4 Quality Education**  
**(Orodha ya Usomaji wa Kiswahili: SDG 4 Elimu Bora)**

## KEN NA KANDI

HADITHI YA WATOTO



ISBN: 978 9976 5 7136 3



MWANAWETU MMUNI


**KICHWA CHA KITABU (Book Title):**  
**MWANDISHI (Author):**  
**MCHAPISHAJI (Publisher):**  
**ISBN:**  
**Lugha (Language):**

KEN NA KANDI (Ken and Kandi)  
MWANAWETU MMUNI  
UCHAPISHAJI WA BINAFSI  
978-9976-5-7136-3  
Kiswahili

## **MAELEZO MAFUPI KUHUSU KITABU KULINGANA NA UN SDG 4 (BRIEF INFORMATION ABOUT THE BOOK ACCORDING TO UN SDG 4)**

Ken na Kandi ni kitabu cha hadithi ya watoto. Hadithi hii imejikita katika mandhari mwafaka ya uwasilishaji. Mwandishi anatumia wahusika wawili ambao wanadhirihisha maudhui kuhusu bidii na elimu maishani licha ya changamoto za maisha. Mhusika mkuu(Ken) anajitahidi masomoni baada ya dadake Kandi kuwacha kutokana na mkosi unaomwandama . Ken anajikakamua hadi kufikia upeo wa elimu yake na kuwa daktari. Elimu ya utabibu anaitumia kumuagua maradhi mwalimu wake aliyekuwa akimdhilisha alipokuwa skuli. Mwalimu Dalila aliamini kwamba watoto hawa akiwemo mhuska mkuu hawakupaswa kusoma katika shule hiyo kutokana na maisha yao ya uchochole yaliyowasakama na kuwaganda. Tamati ya hadithi hii inasawiri funzo kwamba elimu ina nafasi pana ya kubadilisha na kuboresha maisha ya mtu ilimradi hakati tamaa. Hadithi hii inalenga na kufuma lengo la 4(UNSDG4), Elimu bora kwa wote na usawa wa jinsia.

Ken and Kandi are a children's story book. This story is based on the appropriate presentation theme. The author uses two characters who convey content about hard work and education in life despite the challenges of life. Ken is struggling to reach his full potential and become a doctor. He uses medical education to diagnose his abusive teacher when he was in school. The conclusion of this story illustrates the lesson that education has the potential to change and improve a person's life as long as it does not disappoint.




**KICHWA CHA KITABU (Book Title):**  
**MWANDISHI (Author):**  
**MCHAPISHAJI (Publisher):**  
**ISBN:**  
**Website:**  
**Lughu (Language):**

HAKI YANGU (MY RIGHT)  
ESH-NSARIE MARA  
E&D VISION PUBLISHING  
9987 622-89-5  
[www.edvisionpublishing.co.tz](http://www.edvisionpublishing.co.tz)  
Kiswahili

### **HAKI YANGU (MY RIGHT)**

Haki yangu ni kitabu cha watoto chenye maelezo yaliyifungamana katika picha. Picha hizi zimetumiwa kuonyesha jinsi watoto wanapata elimu na mafunzo mbalimbali kuitendo vinavyooneshwa na picha pamoja na maelezo mafupi. Mwanafunzi amepewa wajibu wa kutazama picha au michoro huku akitambua na kusema kinachoendelea katika michoro yenye. Wanafunzi wanajifunza na kuiga vitendo mbalimbali kikiwemo teknolojia ya kisasa. Katika mwisho wa kitabu hiki mna maswali yaliyotungwa pamoja na picha ambazo ambazo ni dira kwa mwanafunzi kufahamu sababu na faida ya kuenda shulen. Mwandishi vilevile ametumia shairi kuwasilisha ujumbe wake kuhusu mtoto kupata haki ya elimu. Haki hii ni mojawapo wa malengo ya UNSDG4 Elimu bora kwa wote na usawa wa jinsia. Fauka ya mwandishi kutumia picha, maswali na shairi kitabu hiki kinaafika kiwango cha watoto wadogo wanaoibukia kufahamu mambo yanahusiana na mazingira yao moja kwa moja.

My right is a children's book with captions attached to the pictures. These pictures have been used to show how children get a variety of education and training through the actions shown in the pictures as well as a brief description. Students learn and imitate a variety of actions, including modern technology. At the end of this book are questions posed along with pictures that are a vision for the student to understand the reasons and benefits of going to school. This right is one of the goals of the UN SDG4 Quality Education for All and Gender Equality. The author uses pictures, questions and poetry. This book reaches the level of young children emerging to understand things that directly relate to their environment.



**KICHWA CHA HADITHI (Book Title):**

HADITHI ZA KARNE YA 21 (21<sup>ST</sup> CENTURY STORIES)

**MWANDISHI (Author):**

MWANAWETU MMUNI

**MCHAPISHAJI (Publisher):**

UCHAPISHAJI WA BINAFSI

**ISBN:**

978-9976-5-7132-5

**Lugha (Language):**

Kiswahili

### **HADITHI ZA KARNE YA 21 (21<sup>ST</sup> CENTURY STORIES)**

Mpangilio wa visa katika kitabu hiki ni maridhawa. Mtiririko wa kila kisa unajitokeza vyema bila mkanganyiko wa vitushi. Visa vilivymo ni vya kusimua. Mfano wa visa vinavyoafikiana na lengo la 4 UNSDG4 kuhusu elimu ni kisa kiitwacho ELIMU MASAFA. Katika kisa hiki mwalimu wa somo la uraia darasa la tano anafundisha wanafunzi kwa njia ya mtandao kutokana na agizo la rais kufunga shule kwa ajili ya Covid 19. Mwandishi anasimulia katika kisa hiki jinsi wanafunzii walivyosoma na kupata elimu kupitia vyombo na mbinu za teknolojia kama vile runinga, kompyuta na nyenzo nyinginezo. Kupitia mifumo hii ya kidijitali wanafunzi wanapata maarifa ya kuepuka homa ya Corona kama vile kunawa mikono, kuvaa barakoa na kuepuka misongamano.

Mbali na kisa cha Masafa Ya Elimu, kisa cha 2 pia mazingira yake yamejikita shulen. Mwandishi anamatumia mwanafunzi wa darasa la 6 ambaye ana ujuzi mwafaka kuhusu manufaa ya mboga na matunda. Ujuzi alioupata baada ya kujifunza shulen. Mhusika aitwaye Mesa ni mwanafunzi anayejibidiisha kupanda na kustawisha mboga za majani na matunda katika bustani yao nyumbani. Ijapo mama anakuwa kizingiti katika juhud za Mesa lakini mwisho anabaini faida ya mboga za majani na matunda. Hali hii inatokana na kuugua kisha daktari

kumweleza ale mboga za majani na matunda kwa wingi. Mamake Mesa anajirudi huku akiomba radhi kuwa kikwazo katika ustawishaji wa bustani ya mboga na matunda. Hatimaye anamuunga mkono na kumpongeza Mesa kwa ajili ya hatua hiyo.

The sequence of stories in this book is multifaceted. The sequence of each story is clear without any confusion. The stories in it are interesting. Fifth grade citizenship teaches students through the internet due to the president's order to close the school for COVID-19. These digital systems students gain knowledge to avoid Corona flu such as hand washing, wearing masks and avoiding congestion.

In addition to the story of the Distance of Education, story 2 is also based on the school. The author uses a 6th grader who has a good knowledge of the benefits of vegetables and fruits. Growing leafy vegetables and fruits in their home garden. Although the mother becomes a threshold in Mesa's efforts but in the end she realizes the benefits of leafy vegetables and fruits. While apologizing for being a hindrance to the development of the vegetable and fruit garden. Finally he supports and congratulates Mesa for the initiative.